JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA UJENZI

# Siku 100 za Vitendo

## na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan







**"Kazi na Utu, Tunasonga Mbele"**


@Wizarayaujenzi
ps@mow.go.tz //www.mow.go.tz

Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 2888, 40470 Dodoma.
Simu: +255 (026) 2324455



## BODI YA UHARIRI:


**Mwenyekiti**
Balozi, Mha. Aisha S. Amour

**Makamu Mwenyekiti**
Dkt. Charles E. Msonde

**Mhariri**
Segolena Francis

**Wajumbe**
Shukuru Senkondo
Deniza Cyprian
Siti Said
Sandra Kiwia
Abdallah Ng'anzi
Ayoub Gota
Dastan Nehemia

**Msanifu Kurasa**
Bolgas Odilo



**Mawasiliano**
Wizara ya Ujenzi,
Mji wa Serikali - Mtumba,
1 Mtaa wa Ujenzi,
S.L.P 2888,
40470 Dodoma.

Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mow.go.tz


## VIONGOZI WAKUU WA WIZARA YA UJENZI



**Mhe. Abdallah H. Ulega (Mb)**
Waziri wa Ujenzi



**Mhe. Mha. Godfrey M. Kasekenya (Mb)**
Naibu Waziri wa Ujenzi



**Balozi, Mha. Aisha S. Amour**
Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi



**Dkt. Charles E. Msonde**
Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Daraja la Mto Pangani lenye urefu wa mita 525 mkoani Tanga.*

# SIKU 100 ZA VITENDO NA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - KAZI NA UTU, TUNASONGA MBELE

Wizara ya Ujenzi ni miongoni mwa Wizara muhimu katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwa na jukumu la kusimamia na kuendeleza Sekta ya Ujenzi ambayo ni nguzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Wizara ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sera na miongozo ya ujenzi, pamoja na ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara, madaraja na majengo ya Serikali. Aidha, Wizara inahakikisha usimamizi wa matengenezo ya mitambo na magari ya Serikali, pamoja na uendeshaji wa vivuko, kwa lengo la kuhakikisha usafiri salama, wa uhakika na unaochochea maendeleo endelevu ya Taifa.

Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu bora, salama na endelevu itakayochochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Aidha, Wizara inasimamia na kudhibiti ubora na usalama wa kazi zote za ujenzi wa barabara, madaraja, vivuko, majengo, mitambo, mifumo ya umeme na vifaa vya kielektroniki, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali huku ikizingatia thamani ya fedha. Kupitia ushirikiano huo, Wizara inakusudia kukuza maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii yanayokidhi mahitaji na matarajio ya serikali na wananchi.

Kwa kulitambua hilo, Serikali imeendelea kuweka misingi imara ya kuhakikisha Sekta ya Ujenzi inakuwa chachu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Watanzania wote, kwa kuzingatia misingi ya usawa, ushirikishwaji na uzalendo wa kiuchumi.

Katika siku 100 za uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imeonesha kwa vitendo kipaumbele cha kulinda na kuzingatia utu wa mwananchi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Kupitia utoaji endelevu wa rasilimali fedha kwa Wizara ya Ujenzi, miradi mbalimbali ya kimkakati imeendelea kutekelezwa kwa kasi na ufanisi, hali iliyoiwezesha Wizara kupiga hatua kubwa katika kuimarisha miundombinu ya Taifa.



*Ujenzi wa Daraja la Pangani lenye urefu wa mita 525 na Barabara unganishi zenye urefu wa Kilomita 25 ukiendelea.*



*Mafundi wakiendelea na ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje yenye urefu wa Kilometa 112.3 mkoani Dodoma.*



*Kazi za ujenzi wa Barabara ya Mabasi yaendayo haraka Awamu ya Nne (BRT IV) ukiendelea mkoani Dar es Salaam .*



*Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega (kushoto) akitoa maelekezo kwa Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam (wa pili kulia) pamoja na Kaimu Mkurugenzi wa TEMESA (kulia)wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani humo. Wa pili kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Balozi, Mha. Aisha Amour.*



*<<<<<<<Muonekano wa barabara eneo la Somanga - Mtama lililoathiriwa kwa mvua za El-Nino za mwaka 2023/24, mkoani Lindi.*

Wizara ya Ujenzi, kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), imekamilisha ujenzi wa miradi 40 kati ya miradi 81 ya madaraja ya dharura inayotekelezwa chini ya programu maalumu ya Contingent Emergency Response Component (CERC), inayofadhiliwa na Benki ya Dunia yenye thamani ya Shilingi Bilioni 500 ambapo utekelezaji wa miradi hiyo imekwenda kutatua changamoto na kuleta tabasamu kwa wananchi.



*Muonekano wa Sehemu ya Barabara ya Mzunguko wa Nje Dodoma yenye urefu wa Kilometa 112.3 inayoendelea kujengwa kwa kiwango cha lami mkoani Dodoma.*

Miradi hiyo ilianzishwa kufuatia athari za mafuriko makubwa yaliyosababishwa na mvua za El Niño pamoja na Kimbunga Hidaya, yaliyotokea kuanzia mwezi Oktoba, 2023 hadi Mei, 2024. Mafuriko hayo yaliathiri miundombinu ya barabara na madaraja katika mikoa mbalimbali nchini, ikiwemo Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Lindi, Rukwa, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Manyara, Geita, Kagera, Shinyanga, Simiyu na Mara.



*Muonekano wa Daraja la Nzali lenye urefu wa Mita 60 ambalo ujenzi wake umekamilika mkoani Dodoma.*

Miradi ya madaraja ya dharura iliyokamilika ni pamoja na Daraja la King'ori (Arusha), Msimbagenge (Pwani), Morena (Dodoma), Fufu (Dodoma), Nzali (Dodoma), Kamishango (Kagera), Katuma (Katavi), Washi (Hedaru-Kilimanjaro).
Mingine ni Daraja la Kipwata (Lindi), Mikereng'ende (Lindi), Mbwemkuru (Lindi), Somanga Mtama (Lindi), Katesh (Manyara), Losinyai (Manyara), Minjingu (Mulungu)- Manyara na Chakwale (Morogoro).



*Muonekano wa sehemu ya Barabara ya Uvinza - Malagarasi Kilometa 51.1 iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hiyo inaunganisha mkoa wa Tabora na Kigoma.*

Aidha, Serikali imesaini mkataba na Benki ya Dunia (World Bank) kwa ajili ya mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Makambako - Songea, Sehemu za Rutukila - Songea na Songea Bypass zenye urefu wa jumla ya kilometa 95.1 kwa gharama ya Shilingi Bilioni 158.67. Taratibu za kuanza kazi za ujenzi zinaendelea.

Sambamba na utekelezaji wa miradi hiyo, Wizara ya Ujenzi imepokea kiasi cha shilingi Bilioni 511.3 kwa ajili kulipa madai ya Makandarasi wa miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini ambapo fedha hizo zinajumuisha fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha Shilingi Bilioni 284.8 na Shilingi Bilioni 226 kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Halikadhalika, Serikali imeyapatia Makampuni manne (4) ya Makandarasi Wanawake Wazawa mradi maalum wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ruanda – Idwiwili yenye urefu wa kilometa 20 Mkoani Songwe. Utekelezaji wa mradi huo unaendelea na umefikia asilimia 10.4 na katika kipindi cha siku 100, Makandarasi hao wamelipwa malipo ya awali yenye jumla ya Shilingi Bilioni 6.818.




*Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wahandisi wakati wa maadhimisho ya saba ya siku ya mafundi sanifu yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam.*

Vilevile, Wizara ya Ujenzi kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), imepata mafanikio makubwa katika kuwawezesha vijana na wanawake kupitia mafunzo kwa vitendo (Structure Engineers Apprenticeship Programme – SEAP). Kupitia programu hiyo, Wahandisi wahitimu watano (05) wamepata mafunzo katika mradi wa kimataifa wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Rumonge – Gitaza na Kabingo – Kasulu – Manyovu.

Aidha, kupitia mradi wa kudhamini wanawake kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway, jumla ya wahandisi wahitimu wanawake 147 wamepata nafasi za mafunzo kwa vitendo katika Taasisi za Umma na Binafsi.



*Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega akipokea tuzo Maalum ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyopewa na Makandarasi kwa kutambua mchango wake katika sekta hiyo nchini.*

Vilevile Katika siku 100, jumla ya Wahitimu 289 katika fani ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi wanaendelea kupatiwa mafunzo ya vitendo kupitia programu ya Archicture and Quantinty Survey Internship Programme (AQIP) inayoratibiwa na Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB).









*Mkurugenzi wa Idara ya Ufundi na Umeme kutoka Wizara ya Ujenzi Qs. Mwanahamisi Kitogo akitoa zawadi wakati wa Mahafali ya pili ya wataalam 170 waliokidhi vigezo vya usajili ambayo yaliandaliwa na Bodi ya Usajili Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB)*

Katika kipindi cha siku 100, serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imetoa jumla ya Shilingi Bilioni 10.278 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Magogoni na MV Kigamboni ambapo ukarabati huo unaendelea.




*Kivuko cha MV Bukondo kikiwa katika maji mara baada ya kukamilika kwa matengenezo yake mkoani Mwanza.*



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Mha. Godfrey Kasekenya akitoa maelekezo wakati akikagua ujenzi wa Darala la Mto Malagarasi linalounganisha Mkoa wa Tabora na Kigoma.*

Katika kipindi hiki cha siku 100, Serikali pia imetoa jumla ya Shilingi Bilioni 20 kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa ajili ya kazi mbalimbali ikiwemo Ujenzi wa nyumba 150 kwa ajili ya makazi ya watumishi wa umma awamu ya pili katika eneo la Nzuguni jijini Dodoma ambapo ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 34;

>>>Ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa (Block C & D) yenye uwezo wa kuchukua familia 32 katika eneo la Magomeni Kota unaendelea na umefikia asilimia 78;

>>>Ujenzi wa Majengo Mawili ya Ghorofa ya Makazi katika eneo la Canadian Village - Masaki jijini Dar es Salaam umekamilika kwa asilimia 95; na



*Ujenzi wa Nyumba za Makazi Magomeni Kota mkoani Dar es salaam*



*Muonekano wa Nyumba za Makazi Masaki, mkoani Dar es Salaam.*



*Ujenzi wa Nyumba za Makazi Canadian - Masaki mkoani Dar es salaam*



*Mradi wa ujenzi wa nyumba za Makazi za Watumishi wa Umma eneo la Nzuguni 'B', mkoani Dodoma.*

Ama kwa hakika, siku 100 za uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan zinaonesha mwelekeo mwema katika miradi ya ujenzi kufuatia mafanikio makubwa na yenye kuonekana katika Sekta ya hii. Utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati unaoendelea katika maeneo tofauti nchini umeimarisha miundombinu, kufungua fursa mpya za kiuchumi na kijamii, na kuboresha maisha ya Watanzania. Kupitia juhudi hizi, Serikali imeendelea kujenga msingi imara wa maendeleo endelevu, ambapo manufaa yake yanamgusa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

**Wizara ya Ujenzi,**
**Mji wa Serikali Mtumba,**
**S.L.P 2888**
**DODOMA.**

**Simu: +255 26 23244455 / +255 26 2322703, 2322702**
**Nukushi: +255 26 2323233 / +255 26 2322704**
**Barua pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mow.go.tz**